JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS.
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na. MDC/S.10/69/VOL.II/07** **10 Septemba, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) ya Magu anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi tatu (03) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II - NAFASI (3)

### 1.1.1 MAJUKUMU

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
iii. Kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine
iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi
v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika
vi. Idara/Kitengo/Sehemu husika
vii. Kukusanya, kutunza na kurejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
viii. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi maandalizi ya vikao mbalimbali
ix. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi

### 1.1.2 SIFA ZA MUOMBAJI.

Kuajiriwa Wahitimu wa kidato cha Nne (IV) wenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha N TA level 6 ya Uhazili. Aidha, wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata program za komputa kama vile• Word, Excel, Powerpoint, Internet, E-mail and Publisher kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS C



CamScanner

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye Mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

iv. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika **Diploma/ Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI,- Computer Certificate, -Vyeti vya Kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards).**

vi. "Testmonial", "Provisional Results ", "Statement of results ", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

vii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE)**.

viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

x. Mwisho wakutuma maombi ya kazi ni tarehe **24 Septemba, 2025.**



CamScanner

xi. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA,**
**1078 BARABARA YA MUSOMA,**
**334021078 ILUNGU,**
**S.L.P. 200,**
**MAGU - MWANZA.**

xii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa Kielekroniki wa Ajira **(Recruitment Portal)** kupitia anuani ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal".

Tangazo hili limetolewa na;

Mohamed Ramadhani
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**MAGU**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MAGU.



CamScanner